

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : press@ikulu.go.tz  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

Ruvuma

26 Septemba, 2024

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameagiza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhakikisha inafufua kiwanda cha kubangua korosho kilichopo Wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, ambacho mwekezaji aliyebinafsishiwa ameshindwa kukiendesha.

Rais Dkt. Samia ametoa agizo hilo leo wakati akihutubia wananchi wa Tunduru katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa CCM wilayani humo.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameagiza viongozi wa Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha kuwa suala la ndovu wanaovamia mashamba ya wananchi katika Wilaya za Namtumbo na Tunduru linashughulikiwa ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao hususan kilimo, wakiwa salama.

Rais Dkt. Samia amewatoa hofu wananchi kuhusu changamoto ya uvamzi wa ndovu na kuwahakikishia kuwa Serikali imechukua hatua stahiki kuhakikisha wanakuwa salama ikiwemo kuweka magari ya doria, kutumia ndege nyuki (*Drone*) ili kuwakimbiza ndovu na kuimarisha vituo vya askari.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia amezindua soko la madini Wilayani Tunduru lililojengwa kwa ubia kati ya wafanyabiashara wa madini na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa, Serikali inatambua mchango wa wachimbaji wadogo wa madini na inaendelea na mipango mbalimbali ya kuwainua ikiwemo kununua mitambo ya kuchoronga madini.

Awali akiwa njiani kuelekea Wilayani Tunduru, Mhe. Rais Dkt. Samia amezungumza na wananchi wa Kata za Lilota, Rwinga na Mchomoro Wilayani Namtumbo pamoja na Tarafa ya Matemanga Wilayani Tunduru.

Sharifa B. Nyanga  
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

